OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA - SONGEA

SHULE YA SEKONDARI RUVUMA
S.L.P. 511,
SONGEA.

14/12/2020

Kumb. Na.RSS/S.30/2/VOL.III/06

Ndugu Mwaanafunzi:

.....................................................................

.....................................................................

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUVUMA KIDATO CHA KWANZA JANUARI -2021

Shule ya sekondari Ruvuma inayoongozwa chini ya utaratibu na miongozo ya serikali, ipo ndani ya Manispaa ya Songea **Km:03** toka katikati ya Mji upande wa kusini mashariki.

**NAPENDA KUKUPONGEZA WEWE** kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule ya sekondari Ruvuma unakaribishwa, KARIBU SANA.

1. **UFUNGUZI WA SHULE**

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** saa **1:00 asubuhi** bila kukosa, masomo ya awali ya lugha ya kiingereza yataanza mara.
**NB:** Mzazi/Mlezi jiepushe na usumbufu usio wa lazima kwa kuzembea kumleta mtoto wako shuleni. (**Angalizo:** kutomleta mwanao shuleni ni kosa la jinai ambalo litakusababishia kifungo)

Pamoja na fomu hii, nimeambatanisha kanuni na sheria za shule pia fomu maalumu ya kupima afya ambapo huduma hii inapatikana **Hospitali ya Mjimwema**, tafadhari zingatia hilo.
**NB:** Mwanafunzi afikapo shule ni lazima afike na hiyo fomu ikiwa imejazwa na daktari baada ya vipimo.

2. **SARE ZA SHULE (UNIFORM)**

**WAVULANA:**

- Shati mbili nyeupe (Plain Tetroni) na Neck - tie. (neck tie iendane na rangi ya suruali )
- Suruali mbili (zisishonwe staili ya modo), ziwe na marinda na turn - up. sampuli ya kitambaa inapatikana shuleni.
- Mkanda wa kufungia suruali usio na marembo
- Viatu vya ngozi - Rangi nyeusi vyenye gidamu (kamba). Visigino vifupi (flat shoes) .
- Socks fupi vyeusi (plain) jozi tatu.
- T-shirt rasmi ya shule rangi ya bluu afike nayo mwenyewe.
- Sweta rangi ya kijani kibichi (jani la mgomba) afike nalo mwenyewe.
- Nguo za michezo., (Bukta na track suit ya blue, Raba, T-shirt) afike nazo mwenyewe.

**WASICHANA**

MKUU WA SHULE
RUVUMA SEKONDARI
S L.P. 511 SONGEA

Scanned with CamScanner

- Shati mbili nyeupe (Plain Tetroni) na Neck - tie. (neck tie iendane na rangi ya sketi )
- Sketi mbili (ziwe ndefu) ziwe na marinda, na sampuli ya kitambaa inapatikana shuleni
- Viatu vya ngozi - Rangi nyeusi vyenye gidamu (kamba). Visigino vifupi (flat shoes) .
- Socks fupi nyeupe (plain) jozi tatu.
- T-shirt rasmi ya shule rangi ya bluu afike nayo mwenyewe.
- Sweta rangi ya kijani kibichi (jani la mgomba) afike nalo mwenyewe.
  Nguo za michezo., (Bukta na track suit ya blue, Raba, T-shirt) afike nazo mwenyewe

MAHITAJI MENGINE

(a) **Masomo darasani**

- Begi la madaftari: Hii ni sehemu ya sare ya shule; kila mwanafunzi lazima awe na mfuko imara wa kuhifadhia na kubebea vitabu na vifaa vingine muhimu vya shuleni.
- Madaftari 15 makubwa (**COUNTERBOOK QUIRE 2 AU QUIRE 3**).
- Kamusi (Dictionary) 1 ya kiingereza kwa kiingereza.
- Peni, rula ndefu (30 cm) na penseli.
- Mkebe (Mathematical set)

(b) **Koti la mvua**

## FOMU ZA DAKTARI NA AHADI YA MZAZI

Fomu ya kupimwa afya ya mwanafunzi imeambatanishwa, hakikisha umepimwa na daktari katika hospitali inayotambulika na serikali na sio kujaziwa fomu, tafadhali uje na fomu hiyo siku ya kuripoti hapa shuleni.

Fomu ya ahadi ya kutekeleza wajibu pamoja na sehemu ya barua inayohusu mzazi wako imeambatanishwa tafadhali fomu zote zikamilishwe na uje nazo hapa shuleni siku ya kuripoti.

## CHETI CHA KUZALIWA

Nakala ya cheti cha kuzaliwa uje nayo siku ya kuripoti shuleni kwani ni muhimu kwa usajili wa mitihani kitaifa na taarifa za shule kwa mwanafunzi wa sekondari na uraia wake.

MKUU WA SHULE
RUVUMA SEKONDARI
S L.P.511 SONGEA

Scanned with CamScanner

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA SONGEA.

SHULE YA SEKONDARI RUVUMA,
S.L.P. 511,
SONGEA.

## KANUNI NA SHERIA ZA SHULE

Kila Mwanafunzi anatakiwa kuzisoma sheria hizi kwa makini azielewe na azitekeleze. Kukiuka sheria hizi kunaweza kukasababisha mambo yasiende ipasavyo hapa shuleni na kuiletea sifa mbaya shule yetu. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya watakaokiuka sheria hizi.

### 1. WANAFUNZI

a) Sharti wasimame na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita au anapoingia mahali walipo wanafunzi.
b) Wasitumie lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
c) Waheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama wazazi wao.
d) Washirikiane, wapendane na wasaidiane wao wenyewe katika mambo mbalimbali.
e) Wathamini na kuziheshimu kazi za aina zote.
f) Wathamini na kuheshimu mali binafsi na mali ya umma.
g) Wathamini muda wa kuwahi katika shughuli zote za shule zilizopo kwenye ratiba ya kila siku. Kila mmoja awahi na ahudhurie wito wa dharula, Waitike wito au ishara ya kuwaita bila kuchelewa.
h) Waheshimu bendera ya taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za taifa.
i) Wanapokuwa darasani, kwenye mikutano, n.k. wanyooshe mikono juu na kusimama wanapoulizwa, au kujibu maswali.
j) Wakaei kimya wakati wote wanapokuwa madarasani. Wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.
k) Waonyeshe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote.

### 2. MWIKO KWA WANAFUNZI

**A. Iwe ni mwiko kwa mwanafunzi kufanya yafuatayo:**

i. Kuvuta sigara ya aina yoyote.
ii. Kushiriki katika aina yoyote ya ulevi.
iii. Kufuga kucha ndefu, kuwa na nywele zisizo katika hali ya usafi, kupaka ina au wanja na kunyoa nyusi.

**B. Iwe mwiko kwa mwanafunzi kufika katika sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:**

i. Chumba cha walimu (staff room) na ofisi zote za shule.
ii. Maabara
iii. Jikoni
iv. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

Scanned with CamScanner

C. Iwe ni mwiko kwa mwanafunzi kutohudhuria:

i. Vipindi vya masomo ndani na nje ya darasa.
ii. Michezo na kazi zozote za mikono
iii. Baraza la shule, kupandisha bendera ya taifa, ukaguzi wa usafi n.k.
iv. Maandalio ya masomo jioni (Preparation)

D. Ni mwiko kabisa kwenda au kuonekana kwenye sehemu zifuatazo:

i. Vilabu vya pombe
ii. Nyumba za starehe
iii. Nyumba za kufikia /kulala wageni (guest house)

## 3. MAKOSA YA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE

i. wizi
ii. Uasherati/uzinzi
iii. Ubakaji
iv. Kupigana au kumpiga mtu mwingine
v. Ulevi wa aina yoyote kama vile bangi, pombe, n.k.
vi. Makosa ya jinai
vii. Uharibifu wa mali ya umma kama majengo, samani (furniture), n.k.
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kudharau bendera ya taifa
x. Kupata mimba au kusababisha mimba
xi. Kutoa mimba
xii. Utoro uliokithiri
xiii. Kumiliki au kuhifadhi simu ya mkononi

MKUU WA SHULE
RUVUMA SEKONDARI
S. L. P. 511 SONGEA

Scanned with CamScanner

SHULE YA SEKONDARI RUVUMA

FOMU INAYOHUSU TAARIFA YA MWANAFUNZI NA MZAZI/ MLEZI

SEHEMU A:

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi ..........................................................................................
2. Tarehe y akuzaliwa ..........................................................................................
3. Dini ..........................................................................................
4. Kabila ..........................................................................................
5. Anuani ..........................................................................................
6. Sahihi ..........................................................................................

SEHEMU B:

TAARIFA YA MZAZI /MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ..........................................................................................
2. Mahusiano yake na mwanafunzi ..........................................................................................
3. Kazi yake ..........................................................................................
4. Anuani ..........................................................................................
5. Namba ya simu ..........................................................................................

Nimesoma na kuelewa maelezo na mahitaji muhimu kwa mwanangu. hivyo kwa ridhaa yangu ninakubali kuwa nitatekeleza yale yanayonihusu kwa wakati.

Jina ..........................................................

Sahihi ....................................................

Tarehe ....................................................

Scanned with CamScanner

## HABARI MUHIMU KWA WANAFUNZI

1. **UGONJWA**

Mwanafunzi anaposhindwa kuhudhuria masomo au shughuli nyingine za shule anapaswa aombe ruhusa kwa makamu mkuu wa shule.

2. **CHETI CHA DAKTARI**

Mwanafunzi lazima aonyeshe cheti cha Daktari wa Serikali kila anapokosa kuhudhuria masomo au shule kutokana na kuumwa.

3. **VIBALI VYA KUENDEA HOSPITALI**

Hivi vinatolewa na mwalimu anayehusika.

4. **MAHUDHURIO**

Haya yatashughulikiwa na walimu, walimu wa madarasa na mwalimu wa zamu

5. **SIMU**

Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga au kusikiliza wala kumiliki simu wawapo shuleni na katika shughuli zote za shule.

6. **OFISI ZA SHULE**

Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia Ofisi za walimu wala nyumba za walimu bila ruhusa.

7. **DARASANI**

Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka darasani bila ruhusa ya mwalimu. endapo mwalimu wa somo hayupo, basi wanafunzi wautumie muda huo kujifunza au kukamilisha kazi walizoachiwa.

Mwanafunzi atatakiwa kufuata sheria zote za shule ipasavyo, akienda kinyume sheria zitachukua mkondo wake.

Asante kwa ushirikiano.

...............................

ALTEMIUS A. KOMBA

**MKUU WA SHULE.**

MKUU WA SHULE
RUVUMA SEKONDARI
S L.P. 511 SONGEA

Scanned with CamScanner

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL,ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES

RUVUMA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 511,
SONGEA
10/12/2019.

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine ........................................................................................................ to her/his physical and mental fitness for admission as a form one ........................................................ student to join secondary school in the year ................................................

......................................................
A.A . KOMBA.
HEADMASTER

The headmaster;
I have examined ........................................................................................ as shown below and consider that she/he is physically and mentally fit/ unfit for admission to pursue a full time secondary school course.

1. Vision with / without glasses, right ........................................ left ..........................................
2. Blood pressure ........................................................ Haemoglobin ........................................
3. Hearing.................................................................................................................................
4. Urine (a) Albumen .................................................. (b) Sugar ................................................
5. Stool ....................................................................................................................................
6. (a) Veneral diseases ................................................ (b) Bilharzias ...........................................
7. Pregnancy ............................................................................................................................
8. Neurosis ...............................................................................................................................
9. Is there any abnormality of :
   (a) The Heart ........................................................................................................................
   (b) The Lungs .......................................................................................................................
   (c) Speech .............................................................................................................................
10. Are there any serious diseases e.g. Leprosy, epilepsy, asthma, diabetes etc.

..................................................................................................................................................
..................................................................................................................................................
..................................................................................................................................................

Date ........................................................ Signature ........................................................
Station ...................................................... Designation ....................................................

MKUU WA SHULE
RUVU... ...UNDARI
S L.P. 511 SONGEA

Scanned with CamScanner